

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



**OFISI YA RAIS TAWALA ZAMIKOA NA
SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA
CHUNYA**



Unapojibutafadhalitaja:

Kumb.Na. CDC/S.10/39/80

Tarehe. 30/6/2023

YAH: TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Chunya anapenda kuwatangazia na kukaribisha maombi ya kazi kutoka kwa waTanzania wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi moja kama ifuatavyo:-

1. MTEKNOLOJIA DARAJA II – Radiografa (Radiolojia)-Nafasi 1

Sifa za Mwombaji:

- Awe amesoma na kuhitimu elimu ya kidato cha nne.
- Awe amesoma na kuhitimu Stashahada katika fani ya Uteknolojia kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali na kusajiliwa na Mabaraza ya Taaluma pale inapohusika.

Kazi/Majukumu ya Kufanya:

- Kuwapima wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi.
- Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi.
- Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality).
- Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa .
- Kusimamia watumishi walio chini yake
- Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
- Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization).
- Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.
- Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

MASHARITI YA JUMLA KWA MWOMBAJI

1. Awe Mtanzania wa umri kati ya miaka 18 – 45.
2. Mwombaji atume barua ya maombi ikiambatana na maelezo binafsi yaliyojitosheleza (Detailed CV) yenye taarifa za sasa na picha tatu(passport size).
3. Maombi yote yatumwe kwenda kwa Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Chunya kwa anuani ifuatayo:-
**Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri ya Wilaya Chunya
S. L. P. 73, CHUNYA.**
4. Barua zote ziwe na anuani sahihi ya mwombaji pamoja na namba za simu zinazopatikana muda wote.
5. Mwombaji aambatishe vyeti vya taaluma na ujuzi.Mwombaji atakayewasilisha '**Result Slip**', '**Statement of Results**', '**Provisional Results**' maombi yake hayatafanyiwa kazi.
6. Mwombaje aweke 'referees' watatu wa kuaminika na wanaopatikana.
7. Kuwasilisha taarifa za uongo/kughushi nyaraka ni kosa la jinai.Hivyo atakayebainika kutenda kosa hilo hatua za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.
8. Waombaji watakaochaguliwa kufanya usaili ndio watakaoitwa kwenye usaili.
9. Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 13/07/2023 saa 9:30 Alasili.

NB:- Nafasi hii inalipwa kwa ngazi ya mshahara wa TGHS B – Tsh 740,000.00 kwa mwezi

Imetolewa na



Athumah M. Bamba

**KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W)
CHUNYA**

**MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
CHUNYA**